**Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama**
**S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: +255-22 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519**
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya kuzalisha umeme kutoka kwa kampuni ya SHANTA MINING COMPANY LTD. EWURA imepitia maombi hayo na inakusudia kuipatia kampuni hiyo leseni ya muda mfupi ili kumwezesha kukamilisha taratibu za kupata leseni ya kuzalisha umeme. Taarifa za mwombaji pamoja na aina ya leseni anayokusudiwa kupewa zimetolewa hapa chini:

| | |
|---|---|
| **1.** | **Jina na Anuani ya Mwombaji**<br>Shanta Mining Company Ltd, S.L.P 79408, Dar es Salaam. |
| **2.** | **Maelezo ya Leseni**<br>a) **Aina ya Leseni:** Leseni ya muda ya kuzalisha Umeme.<br>b) **Madhumuni ya Leseni:** Kukamilisha taratibu za kumwezesha kupata leseni ya kuzalisha umeme.<br>c) **Aina ya Mtambo:** Mtambo wa Megawati 7.5 wa kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta.<br>d) **Aina ya Nishati:** Mafuta mazito (HFO 180).<br>e) **Muda wa Leseni:** Miaka Mitatu (3).<br>f) **Eneo la Mradi:** Kijiji cha Saza kilichopo Wilaya ya Chunya, Mkoa wa Songwe<br>g) **Mteja wa Umeme:** Matumizi Binafsi. |
| **3.** | **Maelezo ya Wanahisa**<br>a) Shanta Gold Holdings Ltd, St Peter Port, Guernsey, GYI 2PU, 99%.<br>b) Shanta Gold Ltd, St Peter Port, Guernsey, GYI 2PU, 01%. |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi tajwa hapo juu awasilishe kwa maandishi maoni yake au pingamizi lake kupitia anuani tajwa hapa chini kabla ya saa 11 jioni, siku ya tarehe 22 mwezi Novemba 2016. Maombi hayo yanaweza kuonyeshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi kupitia anuani hiyo hapo chini kabla ya tarehe 22 Novemba 2016.

**Mkurugenzi Mkuu**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund Towers,
Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama ,
S. L. P 72175, Dar es Salaam
Nukushi: +255 (022) 2923519
Simu: +255 (22) 2923513-18
Barua Pepe: info@ewura.go.tz, Tovuti: www.ewura.go.tz